

Jina :.....Nambari yako:.....

Shule :.....Sahihi:.....

Tarehe :.....

**102/3**

**KISWAHILI**

Karatasi ya tatu

**FASIHI**

MEI/JUNI 2014

MUDA:SAA  $2\frac{1}{2}$

## **MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA EKSIKA**

*Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya(K.C.S.E)*

### **MAAGIZO:**

- a) Jibu maswali manne pekee.
- b) Swali la kwanza ni la lazima
- c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadith fupi na Fasihi simulizi.
- d) Kila swali hubeba alama 20
- e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

## **SEHEMU YA A: USHAIRI**

Linatushangaza, twashangaa dhidi ya kushangaa!

Kwa mangamizi ya kila leo

Tunayotekelezewa na kumbe razini zaidi,

Binadamu!

Hatuui sababu,

Mzinga na mazega yetu kuteketezwa,

Yetu asili kuvinwa kwa mababu na waritimba,

Binadamu wasiojua madhila yetu

Kudamka kutafuta nekta, na kukesha kulinda mzinga!

Lakini kinachotushangaza, twauliza: mwatuchomeani?

Twafedheka jamani!

Masaibu ya tajiri

Tajiri mwema kuwatahirisha wasio na faidha

Badala ya wakatilia moto daraja la fanaka,

Wasijue kesho, kesho kutwa, mtondo.... Watavuna wapi?

Baada ya kutuangamiza, sie vitega chumi vyao.

Tuma haki, kama nyinyi,

Ya kuwaona watoto na wetu vijukuu

Wakikua na kufaidi, jasho letu wazazio

Ingawa hili halijawa faradhi,

Ila kwa mapenzi yenu ya dhati

Kumbuka binadamu,

Hata sisi tuna hisia, tusichomwe,

Japo wajinga tunayo manufaa

Sie hatuwahi, mbona nyie?

Na safari yetu sote, japo njia tofauti.

Twende pole pole!

### **Maswali**

- a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (ala. 2)
- b) Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu. (ala. 4)
- c) Taja na utoe mifano miwili ya tamathali za semi zilizotumiwa katika shairi hili. (ala. 4)
- d) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza idhini za utunzi zinazojitokeza katika tungo. (ala. 4)
- e) Eleza maana ya msamiati ufuatao:
  - i) Razini
  - ii) Masaibu
- f) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (ala. 4)

### **SEHEMU YA B: TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA:**

*Timothy Arege*

- 2. "Hawa ndio watu muhimu katika ulimwengu wa sasa".
  - a) Eleza muktadha wa dondo hili. (ala. 4)
  - b) Fafanua mchango wa mrejelewa katika kusambaratisha baraza la cheneo. (ala. 4)
  - c) Cheneo imekandamizwa kutokana na wakazi wake kutotumia akili.  
Fafanua hii kwa kurejelea tamthilia nazima. (ala. 12)
- 3. Unafiki na tamaa ndio chanzo cha dhiki ya wanacheneo. Thibitisha kwa kurejelea matukio katika tamthilia nzima. (ala. 20)

### **SEHEMU YA C: HADITH FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE:**

*Ken Walibora na Said A. Mohamed*

- 4. Jadili kwa kina maudhui ya uozo wa kijamii na kutowajibika huku ukirejelea hadithi zifuatazo
  - i. Damu nyeusi
  - ii. Maeko
  - iii. Samaki wa nchi za joto

- iv. Kanda la usufi (ala. 20)
5. “Asanteni sana kwa kuja. Sisi kama wazazi na walimu hukabiliana na mengi”.
- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (ala. 4)
  - b) Fafanua matukio yaliyosababisha mkutano huu. (ala. 4)
  - c) Eleza changamoto zozote sita zinazoikumba jinsia ya kike katika hadithi husika. (ala. 12)

#### **SEHEMU YA D:RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA NA Ken Walibora**

6. Moyo ulimpapa na kijasho chembamba kumtekenya juu ya mwanzo wa pua. Akahisi uchungu wa mwiba kujidunga”.
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala. 4)
  - b) Fafanua kwa tafsiri namna mrejelewa alivyojidunga mwiba. (ala. 6)
  - c) Huku ukitumia wahusika wowote wawili eleza namna walivyojidunga mwiba. (ala. 6)
  - d) Tambua na ueleze mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (ala. 4)
7. Taja na ueleze ujumbe muhimu unaojitokeza katika kila barua riwayani. (ala. 20)

#### **SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- 8. a) Eleza tofauti kati ya maghani na mighani. (ala. 2)
- b) Eleza jinsi utakavyowasilisha utanzu wowote wa fasihi simulizi. (ala. 8)
- c) Je, ni vipi jamii ya kisasa inaendeleza fasihi simulizi. (ala. 6)
- d) Eleza mambo manne ambayo huchangia kubadilika kwa fasihi simulizi. (ala. 4)